



**USAID**  
KUTOKA KWA WATU  
WA MAREKANI



## KILIMO

## TANZANIA

Wakati uchumi wa Tanzania ukikua kwa kasi katika muongo mmoja uliopita, zaidi ya asilimia 49 ya Watanzania wanaishi chini ya \$ 1.90 kwa siku (Benki ya Dunia, 2011). Utapiamlo bado uko juu. Zaidi ya asilimia 34 ya watoto chini ya umri wa miaka mitano wamedumaa na karibu asilimia 45 ya wanawake waliofikia umri wa kuzaa wana upungufu wa damu. Ili kusaidia Tanzania kufikia lengo la pili la Maendeleo Endelevu-kutokomeza njaa, kukuza kilimo endelevu, na kuhakikisha kuna upatikanaji wa chakula na lishe bora- USAID inashirikiana kwa karibu na nchi kushughulikia changamoto hizi.

Sekta ya kilimo ya Tanzania - ambayo inachangia karibu theluthi ya Pato la Taifa la nchi na kuajiri asilimia 75 ya idadi ya watu - ina fursa ya kuongeza mapato na kuboresha maisha. Mpango wa Upatikanaji wa Chakula wa Serikali ya Marekani (Feed the Future) unasaidia mipango inayoongozwa na Tanzania, kupunguza umaskini na kuboresha lishe. Feed the Future inatekelezwa sambamba na Mpango wa Uwekezaji wa Nchi ya Tanzania chini ya Programu ya Maendeleo kamili ya Kilimo ya Afrika na Mkakati wa Kitaifa wa Lishe nchini.

Tanzania inaangazia kilimo kama njia bora ya ukuaji wa uchumi. Mipango yake inajumuisha ushirikishwaji wa sekta binafsi ikiwa ni pamoja na Mpango wa Ukuzaji wa Kilimo ukanda wa Kusini mwa Tanzania, ushirikishwaji wa sekta ya umma na sekta binafsi ili kuongeza uwekezaji katika kilimo biashara ndani ya ukanda wa kusini mwa nchi. Feed the Future hufanya uwekezaji unaolenga kusitiza maendeleo ya sekta binafsi ili kuhakikisha uendelevu wa muda mrefu katika kupunguza umasikini na malengo ya lishe. Uwekezaji

## TAARIFA YA KILIMO

### KIWANGO CHA UFADHILI

- Dola za Marekani milioni 5 kwa mwaka wa Fedha 2019

### WASHIRIKI WAKUU

- Wizara ya Kilimo
- Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji
- Wizara ya ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi
- Wizara ya Maji na Umwagiliaji
- Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano
- Ukuaji wa Kilimo Ukanda wa Kusini
- Tanzania Horticulture Association
- ACDI/VOCA
- Africare
- Catholic Relief Services
- CDM Smith
- CGIAR Centers (CIP, ICRAF, IFPRI, IITA)
- Development Alternatives Inc.
- Michigan State University
- Ohio State University
- TechnoServe
- U.S. Department of Agriculture
- U.S. Peace Corps
- Volunteers for Economic Growth Alliance

### MAENEO YA MRADI

Feed the Future Tanzania inaangazia mikoa yenye uwezo mkubwa wa kilimo ambayo hupakana na wilaya zisizo na upatikanaji wa chakula, ikiwemo: Manyara, Dodoma, Morogoro, Iringa, Mbeya, and Zanzibar.

### MAWASILIANO

Andrew Read  
[aread@usaid.gov](mailto:aread@usaid.gov)

### KWA MAWASILIANO ZAIDI

Tovuti: [www.usaid.gov/Tanzania](http://www.usaid.gov/Tanzania)  
Facebook: USAIDTanzania  
Twitter: @USAIDTanzania

huu unasaидia wakulima wadogo wadogo kuwa ushindani zaidi katika uzalishaji na uuzaji wa vyakula vikuu kama vile mchele na mahindi, kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo cha mazao jamii ya mboga (mboga na matunda), na kujenga barabara za zinzounganisha viji ni na barabara kuu ili kuboresha namna ya kufikisha mazao ya wakulima katika masoko.

Ili kuboresha lishe, Feed the Future inakuza utumiaji wa vyakula vyenye lishe bora na mbinu bora za usindikaji wa chakula kama vile una na viini lishe kama madini ya chuma, vitamini A, zinc, na folic acid.

Zaidi ya hayo, uwekezaji wa sekta binafsi na mipango mizuri ya kisera hujenga mazingira wezeshi kibashara na ukuaji wa sekta ya kilimo. Shughuli za utafiti zilizofanywa kwa kushirikiana na taasisi za ndani husaidia kujenga uwezo unaohitajika kwa kilimo endelevu.

## CHANGAMOTO

- Upungufu wa upatikanaji wa rasilimali zenye tija pamoja na fedha, miundombinu dhaifu, na sera dunii hupunguza motisha ya kukuza sekta ya kilimo.
- Uwekezaji wa sekta binafsi katika kilimo unakumbana na uhaba wa mitaji, viwango vya chini vya uwezo na ujuzi wa biashara, na sera zinazokwamisha ukuaji.
- Mabadiliko ya tabia nchi husababisha hatari kubwa ya ukame wa muda mrefu na hali ya hewa isiyotabirika, na kutishia maisha ya jamii ya wakulima wadogo wadogo.
- Ukuaji wa haraka wa idadi ya watu na ukuaji wa kilimo unaleta tishio kwa mali asili ya Tanzania ambayo, ikiposimamiwa vizuri, itasaidia ustawi wa jamii na ukuaji wa kilimo.

## MATOKEO

- **Maboresho katika kilimo:** hektaa zaidi ya 190,000 za ardhi nchini zinatumia teknolojia na mbinubora za kilimo cha kisasa.
- **Faida za Uzalishaji:** Uzalishaji wa mpunga kwa ekari moja kwa wakulima wanaoshiriki umeongezeka kama mara mbili.
- **Unufaikaji wa Sekta:** Watu wasiopungua 450,000 wamenufaika kutokanana mnyororo wa thamani unaoteklezwa Feed the Future.